

JIBU: Yesu ni mtu ambaye alizungukwa na makutano mengi, hivyo isingekuwa rahisi kwao kumkamata wakati wa mchana, kwasababu walijua watakutana na upinzani mkubwa wa makutano.. kama maandiko yanavyosema katika vifungu hivi;

Mathayo 21:45-46

[45]Wakuu wa makuhani na Mafarisayo, waliposikia mifano yake, walitambua ya kuwa anawanenea wao.

[46]Nao walipotafuta kumkamata, waliwaogopa makutano, kwa maana wao walimwona kuwa nabii.

Hivyo njia pekee, ilikuwa ni usiku. Tena wakamwendea na marungu na mapanga kujidai kuwa wanakwenda kumtafuta mwizi, huku miyoni mwao wakijua kabisa wanayekwenda kumfuata ni mtu wa haki.

Na hiyo ni kuthibitisha kwamba walikuwa hawajiamini kwa matendo yao, kwasababu waliyajua ni maovu ndio maana waliyafanya gizani.

Marko 14:48-49

Kwanini Yesu alikamatwa usiku, hawakuyafanya yale mchana?

[48]Yesu akajibu, akawaambia, Je! Ni kama juu ya mnyang'anyi mmetoka wenyepanga na marungu, kunitwaa mimi? [49]Kila siku nalikuwa mbele yenu hekaluni nikifundisha, msinikamate; lakini haya yamekuwa ili maandiko yapate kutimia.

Hiyo ndio sababu kwanini wamfuate usiku, lakini hawakujuua ndio walikuwa wanairahisisha njia ya wokovu. Kufunua kuwa giza kamwe haliwezi kuishinda nuru.

Yohana 1:4-5

[4]Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. [5]Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza.

Mwamini Kristo, Nuru yake ikuangazie moyoni mwako.

Shalom.

Kwanini Yesu alikamatwa usiku, hawakuyafanya yale mchana?

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx1>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

[Bwana Yesu alikufa akiwa na umri gani?](#)

[Yesu kuvishwa taji la miiba kichwani, kulifunua nini?](#)

[Neno I.N.R.I kwenye msalaba wa Yesu maana yake ni nini?](#)

Rudi Nyumbani

Kwanini Yesu alikamatwa usiku, hawakuyafanya yale mchana?

Share on:

WhatsApp